**WATU WANAMSEMAJE MWANDISHI PAMOJA NA KITABU CHA INUKA?**

---

*"Akili kubwa niliyoiona ndani ya Joas nikiwa katika Jopo la usaili wa kazi yake mwaka 2014 ,leo naiona kwa kina zaidi kila nikisomapo kitabu cha INUKA .Hakika Amejikita katika kuwaongoza watu kuziona ,kuzijua na kuzitumia fursa zilizopo ,kutumia mazingira yaliyopo kubuni shughuli ya kipato kuweka watu pamoja ili washirikiane kiuchumi na kuwasimamia waweze kufikia mafanikio yao .Hakika Joas Ameletwa na Mungu ili watu wainuke kiuchumi ".*

***~John J Msonganzila (Mkurugenzi-Tulip General Credit Ltd )***

---

*"Nimemfahamu Joas Yunus tangu nikiwa pamoja nae chuoni chuo kikuu cha Dar es salaam (UDSM) ,ni mtu ambaye amekuwa na shauku kubwa kuona vijana wanainuka na kuchukua hatua madhubuti za kuwaletea mafanikio.Nimepata muda wa kutosha kupitia maandishi yake katika kitabu cha Inuka toleo la kwanza .Hakika ameandika mambo muhimu sana kwa watu wa rika zote ambao wanataka kuona mafanikio katika maisha yao.Kama ningeambiwa nitaje baadhi ya vitabu vya waandishi wa Kiswahili ambavyo vimeandikwa kwa ustadi mkubwa na vyenye uwezo wa kubadili maisha ya mtu ,hakika nisingeacha kutaja kitabu hiki miongoni mwavyo"*

***Kelvin Kitaso (Mkurugenzi-Gracious Printing Press)***

---

*"Kupitia kitabu cha **INUKA,** nimejifunza kushikilia kile ninachokiamini mpaka nione matokeo bila kujali mazingira hasa watu wanaonizunguka .Maneno ninayokumbuka ni kuwa **huwezi kumzuia kuku kutaga** .Ukijiamini hakuna anayeweza kuzuia mafanikio yako.Pamoja na kusoma vitabu vya waandishi wengi kama kitabu cha Tenganamba na vitabu vya Shigongo kitabu cha **INUKA** baada ya kukisoma kimenifanya **ninyanyuke kabisa** kwenda kuitimiza ndoto yangu "*

***Christopher Ndesambulo(Mjasiriamali wa Nafaka –Dar es salaam )***

---

---

*"Joas nilimfahamu kupitia rafiki yangu mwaka mmoja uliopita .Kwangu amekuwa kijana wa njozi zangu .Ana akili ya pekee sana ,ana uwezo mkubwa wa kufikiri ,kuandika na kufundisha.Anajituma ,anapenda sana maendeleo ya wengine na anapenda sana jamii.*

*Kupitia kitabu chake cha **INUKA** na machapisho yake mengi kwa njia ya mtandao ,Joas amekuwa chachu ya mafanikio kwa watu wengi hasa vijana .Kwetu sisi **Clear Future Foundation(CFF**) tumebahatika kwani si tu tunasoma machapisho yake bali pia*

*tumekutana naye na kujadiliana naye .Nakusihi hata wewe unayesoma kitabu hiki ,usinyamaze ,wawezeshe na wengine wakipite ili nao wakombolewe kutoka katika mawazo mgando ya kuona mambo kuwa hayawezekani".*

***AntipacyShinyambala (MBA-Corporate Management)***

***Country Coordinator –Radio Maria&Founder: Clear Future Foundation***

---

*"Namfahamu Joas kama kiongozi na mwanamapinduzi anayepigania ndoto na mafanikio ya wengine kwa kufundisha na kuandika.Licha ya makala nyingi alizoandika kupitia mitandao ya kijamii,INUKA ni kitabu cha kipekee ,kilichobeba nguvu inayoweza kumtoa mtu kutoka chini mpaka juu .Nadhani ni kitabu pekee kilicho katika lugha ya kiswahili nilichokisoma mara nyingi zaidi **."***

***Emamanuel J Kalinga (Sound Mind Coordinator )***

***Founder –Naomba ufanikiwe Initiative***

---

---

*Sina historia ndefu ya kumfahamu ndugu Joas lakini kwa muda wa takribani miaka mitatu ya kufahamiana nae nimemuona ni kijana aliye na ndoto ndefu na watanzania wa hali zote huku akijaribu kuwa na falsafa zinazogusa maisha ya wasomi na wasio wasomi.Mathalani katika kitabu cha INUKA ,jina hili ni uthibitisho tosha wa falsafa ya Joas .Kitabu hiki kimegusia kwa upana wake jinsi gani kila mmoja anatakiwa kupambana ili kuinua hali ya maisha yake mwenyewe.*

***Linus John***

***Mhadhiri Msaidizi chuo kikuu Kishiriki cha Dar es saalam (DUCE)***

---

*"Nimemfahamu Joas kwa miaka kumi na tatu iliyopita .Ni kijana ambaye baada ya kupoteana kwa takribani miaka kumi amepitia kipindi cha mabadiliko makubwa sana .Sina shaka ujumbe wake katika kitabu cha INUKA ni kamili kwa sababu yeye mwenyewe ameweza kwa makusudi kubadilisha hali yake kwa yale anayoandika .Ujumbe wake ni*

*mzito na unaweza kumsaidia mtu mwingine ambaye atausoma na kuamini .INUKA ni tumaini kwa Tanzania na Afrika yetu"*

***Ushindi Elioth –Mwandishi na Kiongozi***

---

*"Unapotaja vijana wachache wa Kitanzania ambao jamii ya ulimwengu inaweza kujivunia ,Joas ni miongoni mwao .Ni mwalimu mzuri wa mabadiliko chanya anayetumia kipaji chake cha uandishi kuwafikishia watu ujumbe unaogonga kengele ya uamusho .*

*Yapo Mengi ya kujifunza toka kwake ,wala huwezi kutilia shaka ujumbe wenye nguvu wa kutia hamasa na kuchochea mabadiliko chanya maishani mwako kutoka katika kitabu chake bora cha **INUKA**"*

***Habel H Samida(Mjasiriamali na mwandishi)***

---

---

*"Joas ni kijana ambaye nilikutana naye katika harakati za kuweza kujenga jamii ya Kitanzania hasa kutoka katika janga la umaskini .Ni kijana mpambanaji anayependa kujifunza ndiyo maana hata kitabu chake cha INUKA kimekuwa kitabu ambacho watu wengi wameweza kubadilisha maisha yao na kutoa shuhuda tele .Ni kijana wa kuigwa kwa anachokifanya kwa kweli "*

***Lazaro Samweli (Mwandishi wa kitabu cha Nguzo tatu za Maisha)***

---

*"Mwandishi wa kitabu cha Inuka Bwana Joas ni Moja ya waandishi bora chipukizi wenye maono na upeo wa kuona mbali .Ni mtu anayeishi na kile anachokiamini na si hivyo tu hutekeleza mipango yake.Kitabu chake cha INUKA hakika kimelenga kumkomboa mtanzania kutoka katika mawazo mgando ya kuamini kuwa kuna mambo yanatakiwa kufanywa na serikali au watu fulani hali inayopelekea wengi kuingia katika dimbwi la ukosefu wa ajira na kuchanganyikiwa lakini ukisoma INUKA inakufungua na kufanya upate tumaini jipya la maisha"*

***F.Kambanyuma(Director DKS Company Ltd & Founder LNF)***

---

*"Kuna wakati nao umekwisha kuwadia ambapo mambo ya kijasiriamali na uchumi ambayo yalikuwa yamefichika miaka mingi sasa yanaibuiliwa katika jamii.Licha ya kwamba Joas nilikuwa namfahamu kwa muda mrefu lakini kinachotoka ndani yake ni*

*kipya kabisa kwangu.Kitabu chake cha INUKA kimenipa nguvu kubwa ya uthubutu hasa katika kuchukua maamuzi ya kiuchumi ya kutengeneza maisha .*

*Kitabu cha INUKA ni uthibitisho wa wazi kwamba wakati umewadia wa kujenga maisha yetu ya kiuchumi bila kutegemea maamuzi ya watu wengine"*

***Vincent Mabula Jilala (CEO Fikia Upeo Company Limited)***

***(Mwandishi wa kitabu cha Mwanzo wa kuwa Tajiri)***

---

**"***Kitabu cha INUKA kilichoandikwa na kijana mwenye kipawa cha pekee ndugu Joas Yunus Buyungu(Jyb) nimekisoma .Hakika kitabu hiki ni moja ya kitabu bora duniani chenye kukuangazia fikra chanya za kukutoa kwenye lindi baya la umasikini.Mimi binafsi amenisaidia na nimefaidika na kitabu ,ni  kitabu cha lazima kukisoma"*

***Mwalimu Adabert Chenche***

---

*"Joas ni mwandishi aliyeona hali halisi ya maisha ilivyo na kuchambua maswala na hali za jamii zetu kwa kiwango cha tofauti sana .Kitabu chake cha INUKA ni daraja kwa vijana wengine KUINUKA na kupiga hatua maishani.*

*Kama neno langu lingekuwa sheria basi hiki ni kitabu muhimu katika maktaba ,shuleni na hata majumbani kwa ajili ya kujikumbusha na kutoa mwongozo wa jamii hasa vijana kuinuka kutoka katika Lindi la umaskini"*

***Raymound Mgeni(Mwandishi wa mashairi)***

---

*"Joas si mwandishi mahiri tu bali pia ni mwalimu ,mhamasishaji na kijana mwenye uchungu zaidi juu ya maumivu yawapatayo watuwote waliopo katika hali duni ya maisha hivyo kupitia kalamu ya Joas,amekuwa ngazi ,amekuwa nuru ,naam,amekuwa chachu ya kuhakikisha  kuwa wewe unainuka na kusonga mbele kimaisha*

*Ni wengi tunaokata tamaa na kujihisi hatuwezi kuinuka tena .Ni wachache wanaojaribu kuinuka pindi wanapogundua kuwa wameanguka lakini wachache zaidi wanaojua maumivu ya kuanguka ,hivyo kuchukua jitahada za kuinuka na kutafuta mbinu za kuwainua wengine wengi zaidi ili kutimiza lengo na kusudio la Mungu  kwa wanadamu.Kitabucha INUKA hakijaniinua tu kutoka nilipokuwa ,bali pia kimenipa nguvu ,mbinu na maarifa ya kufikia malengo yangu na hata kuwainua wengine Kimafanikio"*

***Erick Gamba (Mwalimu na Mwandishi )***

*“Kitabu cha Inuka kilichoandikwa na Joas ni kizuri sana kama unataka kuanza chochote unachokitaka hakikisha umekisoma kitabu hiki ,kama umeshaanza kitabu hiki kitakuwa sababu ya kuinuka pale ulipokwama .”*

***Jacob Mushi***

***Mwandishi wa kitabu cha Siri 7 za kuwa hai leo***

*“Kijana Joas amejikita katika uandishi “halisi” na sio “nadharia” .Anazungumzia maisha halisi na si hadithi za kubuni.Nimemfahamu Joas kwa takribani miaka miwili sasa pale alipotuunganisha katika kundi la “Kijana Jithamini”.Kwa muda huo binafsi nimekuwa nafuatilia mafundisho yake hakika yamejawa na hekima na maarifa makubwa.*

*Kitabu cha INUKA kimemaanisha kuinua fikra za kila atakayechukua hatua kukisoma na kukiweka katika matendo na hakika kitabu hiki chafaa kiwafikie vijana wengi kadri iwezekanavyo.*

*Maudhui ya kitabu ni halisi, na MTU yeyote anaweza kuzifanyia kazi .Ametoa mifano halisi ya Watanzania waliothubutu sambamba na watokao nchi zingine .*

*Natamani kitabu cha INUKA Kingekuwa kwenye mitaala ya mfumo wetu wa elimu ya Sekondari.”*

***Lucien Wilfred (Mwalimu na Meneja wa Kingdom schools)***

*“Namfahamu Joas kama kijana mwenye kupenda kuona vijana wa kitanzania wakifanikiwa zaidi kimaisha kupitia vipaji vyao .Mara nyingi nimeshiriki katika semina mbalimbali za vijana ambazo amekuwa akiziandaa jijini Dar es salaam.Kitabu cha INUKA ni kitabu bora zaidi kwa mafanikio ya vijana na ustawi wa Taifa letu .”*

***Frank Mihayo(Mwandishi na mhamasishaji wa maendeleo***